Biblia Inatufundisha Kuhusu Karama Za Roho

(The Bible Teaches Us About Spiritual Gifts)

Na

Alex Sadat

Biblia Inatufundisha Kuhusu Karama Za Rohoni

Na

Alex Sadat

Juni 26, 2018

Biblia Inatufundisha Kuhusu Karama Za Rohoni

Watu wengi leo wanadai kuwa wana "*karama za roho*" lakini wanashindwa kuelewa kwamba ilikusudiwa kwa ajili ya baadhi ya watu hasa mitume. Marafiki zangu wengi wanadai kuwa wana "*karama za roho"* na nikiwaambia kwenda kuwaponya watu kwenye mahospitali wanashindwa kwa sababu wanafahamu kuwa wanachokifanya ni kuwadanganya watu ili wajipatie pesa. Tunasoma kuhusu "*karama za roho*" ambayo Roho Mtakatifu aliwapa mitume siku ya Pentekoste katika (Mdo. 2). "*Basi ndugu zangu kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu. Mwajua ya kuwa mlipokuwa watu wa mataifa, mlichukuliwa kufuata sanamu zisizonena, kama mlivyoongozwa. Kwa hiyo nawaarifu ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu kusema Yesu amelaaniwa; wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu. Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule. Tena pana tofauti za huduma na Bwana ni yeye yule. Kasha pana tofauti za kutenda kazi bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote. Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo yeye yule; mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.*" (1 Kor. 12:1-11). Kwa maneno mengine, Karama hizi; hekima, maarifa, imani, uponyaji, miujiza, unabii, karama za roho, tafsiri za lugha; wangeweza kupewa watu kwa **kuwawekea mikono ya mitume**, "*Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha,*" (Mdo. 8:17-18). Swali kwa wale wanaodai kuwa wana karama za Roho Mtakatifu; unapata wapi uwezo?

Kwa sababu tunaona kwamba mitume waliwawekea mikono na wakapokea Roho Mtakatifu, mtume ni lazima aweke mkono wake juu ya mtu ili aweze kuwa na uwezo wa Roho Mtakatifu.

Ebu tuwaangalie wale waliobatizwa na kile kilichowatokea. "*Walipoyasikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. Na Paulo alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri.*" (Mdo. 19:5-6). Moja ya sifa ya mtu kuwa naa karama hizi, ni lazima mtume amwekee mikono. Kwa wale wanaodai leo kwamba wana nguvu hizi ni nani amewawekea mikono? Tunamwona Simoni akiwashawishi mitume kwa fedha ili kwamba aweze kuwa na nguvu hizi na ndivyo madhehebu wanafanya. Wanawapumbaza watu na wao wanaamini kwamba wanazo nguvu. (Mdo. 28:8; 1 Tim. 4:14; 2 Tim. 1:6). Watu waliopokea karama hizi za roho WAASINGEWAPA watu wengine (Mdo. 8:5-17). Mitume walipokufa, watu pekee waliokuwa na karama hizi walikuwa ni wale ambao mitume waliwapa. Na watu hao walipofariki karama za roho zilikoma. Ziko wapi leo? Zimekwenda. Na wale wanaodai kuwa nazo leo ni waongo na wachawi. Kuwekewaa mikono ya mitume ilikuwa ndio njia ya pekee ya watu kupata karama hizi. Ndio ambacho Biblia inasema kuhusu swala hili. Kama nilivyosema hapo juu, tunao wale watu "tunaowaita" waponyaji wa imani, wafanya kazi wa miujiza, wanenaji wa lugha, na manabii waongo wanaotabiri mwisho wa dunia, au dhoruba paamoja na wale wanaotafta ishara, miujiza, au maajabu. Unapata wapi uongo huu na upumbavu? Nayaita hivyo kwa sababu ilikoma zamani sana. "*Hatimaye mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*" (Efe. 6:10-12).

Kumb: Roho Mtakatifu walipewa watu wa nyumbani mwa Kornelio ili kuthibitisha kuwa injili ilikuwa kwa ajili ya Mataifa pia, lakini tofauti na mitume hakuna kinachoonyesha kuwa waliwapa Roho Mtakatifu watu wengine au uwezo wao wa kufanya hivyo. "*Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wale wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha , na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu. Ni nani awezaye kuzuia maji hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wakadha.*" (Mdo. 10:44-48). Hawa ndio watu PEKEE ambayo Biblia inatuonyesha mifano miwili inayoonyesha miujiza ya Roho Mtakatifu; mara moja kuanza kwa kanisa na kuwapelekea mataifa injili.